# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com


## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORAKWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu kwa kutujaalia uhai na uzima, ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa lengo la kujadili na kuidhinisha Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutubariki neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake. Aidha, nachukua fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Baraza hili kwa umahiri mkubwa na ninaamini kwamba mtaendelea kuliongoza Baraza hili kwa hekima, busara na uadilifu.

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu, hekima na busara ambapo kumepelekea kupatikana kwa maendeleo pamoja na kuendelea kudumu kwa amani na utulivu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa umahiri na uwezo wake mkubwa ambao umemfanya aweze kudumu

katika wizara hii kwa muda mrefu na kuwajengea watendaji wake uwezo wa hali ya juu wa kiutumishi katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kamati yangu iliridhika na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara hii baada ya kukaa na Watendaji wa Wizara ya Nchi ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora kuichambua na kujadili kifungu kwa kifungu kama taratibu zetu za kikanuni zinavyoelekeza. Kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri wanazozifanya, kwa hakika ni Wajumbe mahiri, wameweza kuijadili Bajaeti hii ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba sasa niwatambue Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora hapo awali ilikuwa ikisimamia mafungu kumi (10) ambayo yakitekeleza programu zote za Wizara hii. Aidha, Kamati inaipongeza na kuishukuru sana Serikali yetu sikivu kwa kuongeza mafungu mapya katika Ofisi hii ikiwemo Fungu G13 Kamisheni ya Wakfu, Fungu G14 Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Fungu G15 Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Pamoja na ongezeko hilo, napenda kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba Fungu A02 la Baraza la Mapinduzi ambalo katika mwaka 2021/2022 lilikua katika Wizara hii limehamishiwa Ofisi ya Rais Ikulu.

FUNGU G 01 OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imeridhishwa na utendaji bora wa Ofisi hii kwa kusimamia vyema majukumu yake pamoja na kuzisimamia Taasisi zote ambazo zinawajibu wa kuwahudumia wananchi katika Nyanja mbali mbali za kisheria, kiuchumi na kijamii. Kwa muda mrefu sasa, Kamati imekuwa ikifuatilia kwa ukaribu sana utendaji wa watumishi wote wa SMZ na kuona mafanikio na changamoto tofauti ambazo zinarudisha nyuma juhudi za watumishi wa umma. Kwa muktadha huo, Kamati inashauri Ofisi iweke utaratibu maalumu utakao wabana wakuu wa Taasisi za Umma ambao hawajawafanyia watendaji wao mafunzo ya awali (induction course) na kuchelewa kuthibitishwa kazini.

FUNGU G 02 MAHAKAMA KUU

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na uamuzi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuona umuhimu wa kuwepo Jaji Mkaazi kisiwani Pemba, jambo ambalo limesaidia sana kupunguza changamoto za uendeshaji wa mashauri ya kesi za haki jinai kwa wananchi wanaoishi Kisiwani Pemba. Licha ya mafanikio hayo Kamati inashauri Mahakama kuimarisha mazingira ya makaazi ya Mheshimiwa Jaji Mkaazi kisiwani Pemba kufanyiwa ukarabati na ununuzi wa samani za nyumba hiyo, kwani nyumba anayoishi kwa sasa haipo katika hali yenye kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, katika mizuunguuko ya ziara zake za kufuatilia taarifa

za utekelezaji wa kazi za bajeti imegundua kuwa majengo mengi ya Mahakama ni machakavu na mabovu ambayo hayafai tena kutumika kwa shughuli za kimahakama kwa kukosa hadhi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia fedha zilizopangwa katika bajeti mpya ya mwaka 2022/2023 kiasi cha Tsh: Bilioni 5.55 zitumike kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati na kujengwa upya kwa Mahakama za Mikoa ikiwemo Mahakama ya Wete, Mahakama ya Konde, Mahakama ya Mkokotoni na Mahakama ya Vuga.

FUNGU G 03 AFISI YA MWANASHERIA MKUU

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza ukomo wa Bajeti ya afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar ambapo ni matumaini yetu kuwa kuongezeka kwa fedha katika fungu hili kutaongeza hamasa ya watendaji kufanya kazi kwa bidii na kujitolea.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inaishauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutumia vyema wataalamu wake ambao wanasimamia mikataba ya Serikali na Taasisi zote za Umma kwani kufanya hivyo kutaisaidia Serikali kuepuka migogoro ya mikataba na kuepusha matumizi makubwa ya fedha ambazo zitatumika kulipia faini za mikataba hiyo pale endapo Serikali itashitakiwa au kulazimika kuvunja mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imepokea malalamiko kadhaa kutoka kwa Taasisi zetu za ulinzi ambazo zimepeleka mikataba yake kwa Mwanasheria Mkuu lakini mikataba hiyo inachelewa kwa kiasi kikubwa na hivyo, kushindwa kutekeleza miradi yao na kukamilisha kwa wakati. Kwa mnasaba huo, Kamati inashauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuhusiana na mikataba ambayo inapelekwa kwake na Taasisi mbali mbali kwa lengo la kuipitia na kuiboresha wahakikishe wameikamilisha kwa wakati na kuipatia

Taasisi husika ili watekeleze miradi yao kwa ufanisi na kuzingatia muda.

## FUNGU G 04 OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imebaini kuwepo kwa changamoto ya kesi nyingi za jinai ambazo zinachelewa kutolewa maamuzi na hivyo kusababisha idadi kubwa ya Mahabusu katika Chuo cha Mafunzo. hali hii inasababishwa na mambo mbali mbali ikiwemo uhaba wa wataalamu wa sheria ambao wanasimamia kesi hizi katika Mahakama zetu. Hivyo, kamati inaiomba Serikali kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa mashtaka kuongeza ajira za wataalamu wa kusimamia na kuendesha kesi hizi ili ziweze kuendeshwa kwa uharaka na kutolewa maamuzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kupitia programu ndogo ya **SG040103** *Operesheni Maalumu zidi ya Makosa ya Udhalilishaji na Dawa za kulevya* Ofisi ya DPP ihakikishe imeandaa mpango maalum utakaowawezesha kupata wanasheria wa kutosha na wenye weledi na masuala ya kesi hizi ili kupunguza uchelewaji wa kesi katika Mahakama zetu pamoja kuhakikisha ushahidi unakalimika kwa wakati kwa mashirikiano yao na Jeshi la Polisi.

## FUNGU G 05 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imeridhishwa na kazi nzuri wanayoifanya ya kuzipitia Sheria zetu na kushauri kwa Taasisi husika ambayo ni Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali namna bora ya kufanya ili sheria zetu ziwe bora na ziendane na wakati. Kwa maana hiyo, Kamati yangu inaishauri Serikali kuwapatia fedha zilizopangwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kiutendaji pamoja na kuimarisha vitendea kazi vya kisasa ambavyo vitarahisisha shughuli zao za kila siku.

FUNGU G 12 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imefarijika sana kuona Taasisi hii sasa imeshapatiwa fungu lake (vote G12) na kujitegemea katika masuala yote ya kifedha. Ni imani ya Kamati hii kwamba maendeleo yao pia yatakua kwa kasi sana kutokana na kuondoka kwa changamoto hii ya muda mrefu. Kamati inashauri Kamisheni kusimamia vyema fungu lake kwa kufikia malengo yaliyopangwa pamoja na kuongeza kasi ya uwajibikaji ili kuendana na wakati tulionao. Aidha, kwa nafasi hii naiomba taasisi hii kufanya juhudi za makusudi za kuwapeleka wafanyakazi wake kupata mafunzo nje ya nchi yanayohusiana na shughuli zote zinazoendeshwa kitaalamu na taasisi zinazohusiana na maasuala ya Wakfu na mali ya Amana.

FUNGU G 13 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali Mtandao (e-Government) ni miongoni mwa taasisi iiliyopata fungu lake (Vote G13) na kuweza kujitegemea kutokana na kupokea ruzuku kutoka Makao Makuu ya Wizara tangu kuanzishwa kwake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Wakala wa Serikali Mtandao kuendelea na utaratibu wa kuzipitia Taasisi zote za Umma na kuwaunga katika mifumo ya mawasiliano ya kiserikali ili kuepusha Taasisi hizi kutumia mifumo ambayo ipo nje ya Serikali na hivyo, kupelekea taarifa nyingi za Serikali kuvuja na kuhatarisha usalama wa nchi yetu. Sambamba na hilo, tunaiomba Serikali ihakikishe imeipatia wakala fedha zitazoidhinishwa pamoja na kununua vifaa vya kisasa ili kwenda sambamba na mabadiliko ya Ulimwengu katika teknolojia ya habari na mawasiliano.

FUNGU G 14 OFISI YA MUFTI MKUU WA ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu sana Baraza hili Tukufu limekuwa likipigania

kupatikana kwa fungu la Ofisi ya Mufti ambapo kwa mwaka huu tumeona jambo hili likifanikiwa na hivyo Kamati tunatoa pongezi za dhati kabisa kwa Serikali kwa kuweka fungu hili kwa kuzingatia umuhimu wake katika nchi yetu. Kwa kuwa dhamira kuu ya Ofisi hii ni kukuza uadilifu, ufanisi katika kutoa fatwa, utatuzi wa migogoro na kusimamia mambo ya kiislamu. Ni matumaini yetu kwamba dhamira hii itafikiwa pale ambapo fedha za uendeshaji kupitia programu kuu ya PG 1402 *Utawala na Uendeshaji* zitaingizwa na kutumika inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini changamoto kubwa ya uhaba wa nafasi za kufanyia kazi, uhaba wa wataalamu wa fani mbali mbali za dini ya Kiislamu na uhaba wa vyombo vya usafiri; changamoto hizi zipo kwa muda mrefu hivyo, tunategemea kupitia Bajeti hii changamoto hizi zitaondoka kwa kutumia fedha ambazo wametengewa kwa mujibu wa Bajeti yao.

FUNGU G 15 TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ZANZIBAR

Mheshimiwa Spika, Tume ya Maadili ya Viongozi imedhamiria kukuza tabia na vitendo vyenye kufuata maadili kwa viongozi wa Umma kwa kuimarisha uwazi, uwajibikaji, utii na usimamizi wa sheria. Licha ya kuwa na dhamira nzuri yenye kuonesha dira ya mafanikio, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya kukosekana kwa uelewa wa kutosha kuhusu masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa baadhi ya wananchi na baadhi ya viongozi wapya na waliopo katika mfumo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kupitia Taasisi hii ambayo nayo imepewa fungu lake na kujitegemea ikasimamie vyema fedha zitakazoidhinishwa katika kutekeleza programu zake mbali mbali ikiwemo programu ndogo ya Utawala, Mipango na Rasilimali Watu; kwa kuajiri wataalamu pamoja na kusimamia utatuzi wa changamoto ya usafiri kwa Unguja na Pemba.

FUNGU E 05 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar ni Taasisi moja wapo ambayo inajenga dhana kuu ya uwepo wa mfumo wa Utawala Bora na Muundo wa Serikali uliowazi wenye Uwajibikaji na Kupingana na Vitendo vya Rushwa katika uchumi wetu. Sambamba na hilo, Mamlaka hii imesaidia sana kupunguza vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi katika maeneo mbali mbali kutokana na elimu bora ya mapambano dhidi ya rushwa iliyojengwa katika jamii.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya majengo ya ofisi za Mamlaka katika Mikoa na Wilaya na hivyo kupelekea baadhi ya maeneo kutofanya kazi zao kwa ufanisi. Kamati inashauri Serikali kulishughulikia suala hili kwani kuboreshwa kwa Ofisi za Mamlaka kutazidisha ari ya uwajibikaji na moyo wa kujitolea kwa watendaji. Sambamba na hayo, Kamati inaishauri ZAECA kwasasa kuitumia ofisi za Kinyasini Mkoa wa Kaskazini Pemba kama Makao Makuu ya Mamlaka kwa upande wa Pemba kutokana na changamoto ya ofisi kuu iliyopo Chake-Chake. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu na unyeti wa mamlaka hiyo kamati inashauri, Serikali kuharakisha taratibu za kuwapatia jengo jipya na lenye hadhi ya Mamlaka hii.

FUNGU E 07 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

**Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utumishi wa Umma ina lengo la kuimarisha mifumo ya rasilimali watu katika utumishi wa Umma, lengo ambalo litapelekea kuwepo kwa uwajibikaji kwa watumishi katika kutii sheria, kanuni na taratibu katika utumishi wa Umma. Aidha, Kamati inasikitishwa na baadhi ya Taasisi kupitia watendaji wake kushindwa kutekeleza vyema lengo hilo huku wakiifanya jamii kukosa Imani na huduma zinazotolewa katika Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia prohgramu kuu ya PE 0701 *Usimamizi wa Utumishi wa Umma;* Kamati inashauri Kamisheni kufuatilia kikamilifu na kuwachukulia hatua watendaji wote ambao wanakiuka sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma kwa

kuwanyanyasa wananchi wakati wanapofika kupatiwa huduma kwani tabia hii si njema na ni miongoni mwa maadili mabaya kwa watumishi wa Umma katika kujenga Utawala Bora. Kamati inashauri kuwapa mafunzo ya mara kwa mara yatayohusu namna bora ya kuwapatia huduma wananchi wanapofika kupatiwa huduma katika taasisi zetu.

FUNGU E 08 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

**Mheshimiwa Spika,**Kamati inapongeza Tume ya Utumishi Serikalini kwa kusimamia vyema wajibu wao na kuhakikisha kila mtumishi amepata haki yake stahiki. Kwa kuwa Taasisi hii ina programu inayosimamia Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini, Kamati yangu inashauri haki za watumishi zisimamiwe kikamilifu kila mmoja apate haki yake kwa mujibu wa nafasi na taasisi anayoitumikia kwa watumishi wote wa kudumu na wale wa mikataba ya muda mfupi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Taasisi hii kufanya utafiti wa kina kwa taasisi zote za Serikali na kuona changamoto iliyopo katika utendaji pamoja na mapungufu makubwa ya watumishi ambayo yanaathiri maendeleo ya taasisi hizo. Kamati pia inaiomba Serikali kujaza mapengo ya watumishi wanaostaafu kwa wakati muafaka ili kazi ziendelee kwa ufanisi zaidi.

HITIMISHO NA MAONI YA JUMLA KWA ORKSUUUB

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kuchukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu, kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kama zilivyopangwa ili ufanisi wa kiutendaji uweze

kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kamati katika ufatiliaji wa kazi zake imebaini kwamba kuna changamoto kubwa katika utekelezaji wa Sheria Nam. 7 ya mwaka 2018 hali ambayo imesababisha vijana wengi wa kiume kuwekwa mahabusu kwa muda mrefu hivyo kuhatarisha maisha yao na ustawi wa jamii kwa ujumla. kamati inaishauri Serikali kuifanyia mapitio Sheria hiyo ili kuondoa changamoto hizo.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa,Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie vyema Bajeti hii na hatimae waiidhinishie Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha zilizopangwa kutumika katika mwaka wa fedha *2022/2023* ili wapate kutekeleza majukumu yao ambayo ndio msingi mkuu wa Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu*Naomba Kuunga Mkono Hoja.*

Ahsante,

……………….……………..

(Machano Othman Said)

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa**

BARAZA LA WAWAKILISHI,

<u>ZANZIBAR</u>